TANGAZO LA SERIKALI NA.553 la tarehe 26/7/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (1)(d))*

AMRI LA MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MAKAMBAKO (“MAKAMBAKO WSSA”), 2019

Jina la Amri

1. Amri itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako (“MAKAMBAKO WSSA”), (ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Amri hii itachukuliwa imeanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Julai 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Makambako (Water Supply and Sanitation Authority) zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) ifikapo tarehe 31 Oktoba 2019 au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili;

(b) Mamaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako ihakikishe kuwa inazingatia matakwa ya kukusanya tozo ya udhibiti na kuiwasilisha EWURA;

(c) ifikapo tarehe 31 Oktoba au Kabla, Mamlaka ya majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako iandae mpango wake wa kila

mwaka wa kuwatembelea wateja na kuijulisha EWURA kuhusu mpango huo;

(d) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(e) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(f) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne;

(g) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako katika siku zijazo.

Utenguzi wa Tangazo la Seriakali .Na. 472 la 2017

5. Amri hii inafuta matumizi ya Amri Na. 2017-004 ya mwaka 2017 katika maeneo yanayo hudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako.

## MAJEDWALI

### JEDWALI LA KWANZA: BEI NA ADA ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba (a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Aina ya Mteja | Bei za Sasa | Bei iliyopendekezwa | | | Bei iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 580 | 1,140 | 1,269 | 1,422 | 1,000 | 1,100 | 1,300 |
| Taasisi | 730 | 1,431 | 1,592 | 1,784 | 1,400 | 1,500 | 1,700 |
| Biashara | 745 | 1,466 | 1,631 | 1,828 | 1,400 | 1,500 | 1,700 |
| Viwandani | 1045 | 2,048 | 2,279 | 2,553 | 2,000 | 2,200 | 2,400 |
| Magati | 500 | 1,164 | 1,295 | 1,451 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| Ujenzi | 1,460 | 2,862 | 3,185 | 3,568 | 2,000 | 3,000 | 3,000 |

Jedwali Namba (b): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada yasasa | Ada Zilizopendekezwa | | | Ada zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/19 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Wateja Wote | Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi | Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi | | | Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi kama ilivyobainishwa katika Kanuni za Maji safi za mwaka 2013 | | |

Jedwali Namba (c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Ada Zilizopendekezwa | | | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Domestic | 16,000 | 25,000 | 30,000 | 35,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Institution | 22,000 | 35,000 | 40,000 | 45,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Commercial | 22,000 | 35,000 | 40,000 | 45,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Kiosk | 22,000 | 35,000 | 40,000 | 45,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Constructions | 22,000 | 35,000 | 40,000 | 45,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Industrial | 22,000 | 35,000 | 40,000 | 45,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| MaelezoyaKazi | TZS (milioni) | | | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | |
| Matengenezo | | | | |
| Matengenezo ya sehemu ya bomba kubwa la Fukulwa kutoka Mtwango hadi Makambako(Mwaka wa 2019/20 0.402km eneo la Ilunda, Nzivana Emerberg Area , Mwaka 2020/21 urefu wa 0.126km eneo la Korogo la wanajeshi na Korongo la Mtati, Mwaka 2021/22 urefuwa 0.108km eneo la Mbugani) | 67.00 | 31.5 | 31.5 | Itatekelezwa kufikia tarehe 30 Juni 2022 |
| Ununuzi na kufunga dira za wateja pamoja na dira kubwa (water meters & Bulk water meters) | 21.8 | 10.2 | 6.7 | Itatekelezwa kufikia tarehe 30 Juni 2022 |

| MaelezoyaKazi | TZS (milioni) | | | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | |
| Matengenezo | | | | |
| Jumlandogo (Ukarabati ) | 88.8 | 41.7 | 38.2 | |
| UwekezajiMpya | | | | |
| Ujenzi wa Mabomba ya Usambazaji kutoka tanki jipya la Mizani hadi mtaa wa Maguva ni umbaliwa km 9.4. | 250 | 200 | | Itatekelezwa kufikia tarehe 30 Juni 2021 |
| Ujenzi wa kuga wa vyumba kwenye jingo jipya la ofisi pamoja na kununua vifaa vya office, vifaa vya maabara na pikipiki | 138.1 | | | Itatekelezwa kufikia tarehe 30 Juni 2020 |
| Jumlandogo - (Uwekezajimpya) | 388.1 | 200 | | |
| Jumla ya Gharama za Uwekezaji | 476.9 | 241.7 | 38.2 | |

JEDWALI LA TATU
VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Description | Unit | Perfomance Target | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Kiwango cha idadi ya watu wanaoishi katika eneo lililofikiwa na mtandao wa maji | % | 70 | 72 | 74 |
| Kiwango cha asilimia ya idadi ya watu wanao hudumiwa na Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Makambako | % | 65 | 66 | 68 |
| Kiwango cha upotevu wa maji (NRW) | % | 25 | 24 | 23 |
| Wastani wa saa za huduma | % | 16 | 18 | 20 |

JEDWALI LA NNE
MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA

| Gharama | 2019/20 | | 2020/21 | | 2021/22 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Iliyopendekezwa | Iliyoidhinishwa | Iliyopendekezwa | Iliyoidhinishwa | Iliyopendekezwa | Iliyoidhinishwa |
| Uzalishaji | 77.70 | 77.70 | 81.70 | 81.70 | 86.20 | 86.20 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Usambazaji | 184.4 | 184.4 | 179.0 | 193.62 | 184.40 | 203.30 |
| Matengenezo | .5072 | 72.50 | 76.10 | 76.10 | 79.90 | 79.90 |
| Watumishi | 291.00 | 291.00 | 345.10 | 345.10 | 419.70 | 419.70 |
| Utawala | 398.70 | 184.11 | 422.70 | 193.32 | 445.60 | 202.99 |
| Matangazo | 4.10 | 4.10 | 4.60 | 4.60 | 5.00 | 5.00 |
| Matukio na Uchangiaji | 7.50 | 7.50 | 8.30 | 8.30 | 9.20 | 9.20 |
| Bodi | 27.10 | 27.10 | 28.40 | 28.40 | 29.80 | 29.80 |
| Fedha | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| JumlayaUendeshajinaMatengenezo | 1,063.0 | 848.41 | 1,160.5 | 931.14 | 1,259.8 | 1,036.1 |
| Uchakavu | 157.80 | 157.80 | 213.50 | 213.50 | 260.00 | 260.00 |
| FiadayaUwekezaji | | 124.84 | | 137.79 | | 148.34 |
| Jumla ya Mahitaji ya Fedha | | 1,288.76 | | 1,495.9 | | 1,705.4 |
| OndoaMapatoMengine | | 41.900 | | 44.90 | | 45.50 |
| Mahitaji ya Fedha kutoka Mauzo ya Maji | | 1,246.8 | | 1,451.0 | | 1,659.9 |

Dodoma
………………, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*